



# Virusi vya Hanta (Hantavirus)

Karatasi ya Maelezo



Virusi vya hanta ni kundi la virusi ambavyo huenezwa hasa na panya wa aina fulani. Nchini Marekani, hawa ni pamoja na baadhi ya panya wa aina mbalimbali. Maambukizi ya virusi vya hanta yanaweza kusababisha dalili mbalimbali.



Virusi vya Hanta huenea kwa kuvuta hewa yenye mate, mkojo, kinyesi, au mabaki ya viota vya panya walioambukizwa ambayo yamesambaa hewani. Ni nadra sana kuumwa na panya kusababisha virusi vya hanta. Mara nyingi ugonjwa huu hauenei kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine.

## Dalili na Ishara



Homa na Kutetemeka



Maumivu ya Misuli



Maumivu ya kichwa



Kichefuchefu na Kutapika



Kuharisha



Kikohozi

Dalili zinaweza pia kujumuisha kizunguzungu. Katika hali mbaya, kuishiwa na hewa na kikohozi vinaweza kusababisha kujaa kwa maji kwenye mapafu na ukosefu mkubwa wa oksijeni mwilini. Kwa kawaida dalili huanza kuonekana wiki moja hadi nane baada ya kugusana na virusi.



Zungumza na mtoa huduma wako wa afya ikiwa utapata yoyote ya ishara na dalili hizi baada ya kugusana na panya. Hakuna matibabu kwa virusi vya hanta.

# Zuia Virusi vya Hanta

Njia bora ya kuzuia virusi vya hanta ni kuondoa vyanzo vya chakula, maji, na vitu ambavyo vinatoa mahali pa kuishi kwa panya.



## Ziba Matundu

Ziba matundu au nyufa zote ndani na nje ya nyumba



## Tega Mitego

Tumia mitego ya kunasa kukamata panya wakubwa na wadogo



## Safisha Mazingira

Ondoa vyanzo vyote vya chakula vya panya

## Ili kusafisha mabaki ya panya:



Fungua milango na madirisha ili kuruhusu hewa safi iingie kwa angalau dakika 30 **kabla** ya kuanza kusafisha eneo hilo



Vaa glovu na barakoa ya kuzuia vumbi **kabla** ya kuanza kusafisha



Usitumie kamwe kifyonza vumbi au ufagio kusafisha kinyesi au masalia ya viota vya panya



Nyunyizia kinyesi cha panya mchanganyiko wa klorini na maji na kisha tumia taulo ya karatasi kuokota mkojo na kinyesi hicho

## Kwa Taarifa Zaidi, Tembelea:



1. [www.maine.gov/dhhs/hantavirus](http://www.maine.gov/dhhs/hantavirus)
2. [www.cdc.gov/hantavirus](http://www.cdc.gov/hantavirus)
3. [www.cdc.gov/healthy-pets/rodent-control/](http://www.cdc.gov/healthy-pets/rodent-control/)

Unaweza pia kupigia simu Maine CDC kwa 1-800-821-5821.